# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


## MUKHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, sifa njema zote ni zake Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, ambae ametujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kukutana hapa leo, kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa nimesimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Mukhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kwa mwaka 2021/2022 kama ambayo Kanuni ya 109(15) ya Baraza lako Tukufu, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika,kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya PAC ilizifanyia kazi Ripoti tano kama zifuatazo:-

i. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30Juni,2020.

ii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018

iii. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2020

iv. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018

v. Ripoti ya Ukaguzi Maalum Unaohusu Utekelezaji wa Maagizo ya Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Hussein Ali Hassan Mwinyi wakati wa kuwaapisha Viongozi Wakuuu unaohusu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) imezifanyia kazi Ripoti tano za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo ndizo msingi mkuu wa kazi za Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC kwa kipindi hiki haikuweza kuzifanyia kazi Ripoti zote za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa katika Mkutano wa pili wa Baraza la kumi kikao cha tarehe 10 Febuari 2021 ikiwemo Ripoti ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2020 na pia imechukua baadhi ya maeneo katika Ripoti ya Ukaguzi Maalum unaohusu Utekelezeji wa Maagizo ya Raisi wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Mhe Dkt Hussein Ali Mwinyi wakati wa kuwaapisha Viongozi Wakuu.Hata hivyo, Ripoti hizo zinatarajiwa kufanyiwa kazi katika mzunguko ujao wa kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzifanyia kazi Ripoti hizo Kamati imefanya kazi zake kwa mashirikiano makubwa na Mawizara na Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Kamati za Mfuko wa Jimbo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida Kamati ya PAC hufanya kazi zake moja kwa moja na watendaji wa Mawizara na Taasisi za Serikali wakiongozwa na Makatibu Wakuu au Wakuu wa Taasisi ambao ndio wenye dhamana ya vifungu vya fedha katika Wizara na Taasisi zao.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kwa baadhi ya wakati Kamati pia ilikuwa ikifanya kazi na Mawaziri ambao hushiriki katika kazi za Kamati ili kuona uwajibikaji na masuala ya kifedha yanavyoendeshwa katika Wizara wanazozisimamia pamoja na changamoto zake.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua na kuthamini ushiriki wao katika kazi za Kamati, kwa niaba ya Kamati ya PAC, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukurani kwa

Mawaziri wote walioshiriki katika kazi za Kamati yetu kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, aidha katika kufanya uchunguzi wake, Kamati ya PAC ilitumia njia kuu tatu zifuatazo.

1. Kufanya vikao vya mahojiano na watendaji mbalimbali wa Serikali pamoja na Kamati za Mfuko wa Jimbo.
2. Kukagua nyaraka na vielelezo vilivyohusika na hoja zilizojadiliwa (Compliance Audit).
3. Kufanya ziara katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ili kuweza kujiridhisha na kuthibitisha juu ya utekelezaji unaohusika na kuangalia iwapo matumizi ya Serikali yamezingatia thamani halisi ya fedha (value for money audit).

Mheshimiwa Spika, tathmini ya Kamati ya PAC inaonesha kuwa Wizara na Taasisi za Serikali zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali katika kurekebisha dosari za kiutendaji zinazobainishwa na vyombo vya Uchunguzi na Udhibiti wa Hesabu za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Kamati ya PAC. Hivyo, kipo kiwango cha kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa mapato na matumizi „Kamati ya PAC imebaini kuwa licha ya kuimarika kwa utendaji na nidhamu ya matumizi ya rasilimali za umma katika Serikali, yapo pia mambo kadhaa ambayo Serikali inahitaji kuongeza jitihada za kuyafanyia kazi ili utekelezaji wa mipango ya Serikali uende sambamba na utii wa Sheria, Kanuni, na taratibu zilizopo zikiwemo zile zinazoongoza masuala ya fedha na ununuzi katika Serikali.

Mheshimiwa Spika, Katika Ripoti za Ukaguzi za Mawizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na 2017/2018 Kamati ya PAC imebaini mambo makubwa yafuatayo :-

1. Kukosekana kwa mashirikiano ya Watendaji ndani ya Mawizara na Taasisi zenyewe na Ushirikiano baina Mawizara na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Serikali .

2. Uwekaji mbaya wa kumbukumbu za mapato na matumizi.
3. Utekelezaji na Usimamizi mbovu wa Miradi ya Serikali.
4. Kukosekana kwa uhalisia wa nyanzo vya mapato.
5. Matumizi mabaya ya fedha za Serikali (mradi wa visima)
6. Madeni ya muda mrefu.
7. Ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za Ununuazi

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la kukosekana kwa ushirikiano, Kamati ya PAC imebaini kuwa wakati Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mthibiti wanapofanya ukaguzi wanakuwa hawapati ushirikiano wa kutosha kutoka kwa baadhi Watendaji ndani ya Mawazara na Taasisi za Serikali, kwa mfano, wakati Kamati ilipokuwa Chuo cha Mafunzo ikifuatilia Hoja Namba 5.2.3.5 inayohusu matumizi ya fedha bila ya kuwa na mkataba shilingi 173,641,325 .

**Mheshimiwa Spika,** kushindwa kwa watendaji wa Chuo cha Mafunzo kuwapatia ushirikiano wakaguzi kwa kukosa kuwapa Mkataba wa Chuo cha Mafunzo na ZIPA ambao ulikuwemo ndani ya Ofisi kumepelekea kuingizwa hoja hii katika kitabu cha Ripoti ya Mkaguzi huku ikiwaacha Viongozi Waandamizi wa Chuo hicho waliousamimia Mkataba huo wakiwa wameshangaa.

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo la mapato, Kamati imebaini kuwa bado kuna haja kubwa kwa Serikali kufanya tathmini na tafiti za kina juu ya vyanzo vyake vya mapato ili mipango na bajeti ya Serikali katika mapato iendane na hali halisi na uwezo wa vyanzo hivyo katika kutoa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** inaonekana zipo baadhi ya Taasisi za Serikali zinakusanya fedha nyingi lakini hazichangii chochote katika Mfuko Mkuu wa Serikali na zipo nyengine zinaonekana kuwekewa makadirio madogo ya kuchangia Serikalini wakati uwezo wao wa kukusanya ni mkubwa.Halkadhalika zipo pia Taasisi zinapangiwa makadirio

makubwa ya kukusanya lakini uwezo wao ni mdogo.

**Mheshimiwa Spika,**kwa upande wa Utekelezaji na Usimamizi mbovu wa Miradi ya Serikali ,Kamati ya PAC imebaini kuwa katika Mradi wa Kilimo uliokuwa baina ya Wizara ya Vijana, Utamaduni,Sanaa na Michezo ambapo Wizara hiyo iliingia Mkataba na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) wenye thamani ya shilingi 528,612,000 kwa ajili ya ujenzi wa Vitalu nyumba(Green house)19 kwa Unguja na Pemba na uchimbaji wa visima 32(Unguja na Pemba).Katika Mradi huu Serikali ilikuwa ina nia njema ya kuwasaidia vijana katika kuwapatia ajira katika shughuli za kilimo

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ya PAC inasikitika kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa lengo na tija iliyookusudiwa katika Mradi huu haijafikiwa na badala yake fedha za Serikali zinaonekana kutumiwa vibaya na kupotea ''kwa lugha ya kileo tunasema fedha hizi zimepingwa''

**Mheshimiwa Spika,** Katika kufuatilia mradi huu ulioanishwa katika Hoja namba 5.14.1.2 iliyomo katika Ripoti ya Mdhiti inayohusu kasoro katika utekelezaji wa mradi wa Kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kamati ya PAC imefanya ziara mbali mbali katika maeneo ya Mradi huu ya Unguja na Pemba ili kujionea hali halisi ya utekelezaji wa Mradi na katika uchunguzi wake Kamati imebaini dosari zifuatazo:-

i. Kutokamilika kwa Mradi na muda uliowekwa umeshapita.

ii. Zaidi ya asilimia 90 ya Visima na Vitalu nyumba havifanyi kazi

iii. Ukiukwaji wa masharti ya Mkataba ambapo fedha zote za Mradi zimeshalipwa wakati mradi haujakamilika na wala haujakabidhiwa pamoja na kukiukwaji wa vipengele vya ujenzi vya Mkataba huo.

iv. Mradi wa uchimbaji Visima kupewa Taasisi isiyokuwa na utaalam na uzoefu wa kazi hiyo.

v. Mradi kuonekana kutofanyiwa upembuzi yakinifu kwa umakini ambapo Mradi umeainisha kuchimbwa visima vya makalbi wakati baadhi ya maeneo hayafai kuchimbwa visima vya aina hiyo, hata ujenzi wa vitalu nyumba (green house) haukuzingatia vigezo vya kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shilingi 528,612,000 zilizofujwa ni fedha nyingi za Serikali, Kamati ya PAC inashauri Serikali kuwachukulia hatua wale wote waliohusika kwa namna moja au nyengine na uharibufu na ufujaji huo mkubwa wa fedha za Serikali. Aidha Kamati ya PAC inashauri Wizara na Taasisi za Serikali kufanya utafiti wa kutosha (due diligence) kwa Kampuni au Taasisi kabla hazijawapa kazi ili kujua uwezo wa kampuni hizo kwa lengo la kuepusha kuitia hasara Serikali.

Mheshimiwa Spika,Kamati ya PAC inatambua kwa kina hatua ambazo Serikali inachukua katika suala zima la kuhakikisha watumishi wake wanapata stahiki zao,lakini Kamati ya PAC imebaini kuwa bado kuna baadhi ya Wizara yapo Madeni ya muda mrefu ya malipo ya Fidia kwa Watumishi waliopata ajali wakiwa kazini hali hii imebainika katika iliyokuwa Wizara ya kazi, Uwezeshaji,Wazee,Wanawake na Watoto kwa kupitia kitengo cha fidia ambacho kwa sasa kipo chini ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika,Hadi mwezi Januari 2021 wakati Kamati ilipokuwa inafuatilia hoja namba 3.13.14 inayohusu madeni ya muda mrefu yanayotokana na ulipwaji fidia jumla ya shilingi 58,789,503 zinazotokana na watumishi waliopata ajali wakiwa kazini. jumla ya watumishi 33 walikuwa bado hawajalipwa fidia kwa upande wa Unguja. Aidha kwa upande wa Pemba jumla ya watumishi 18 wa Wizara na Taasisi za mbalimbali za Serikali walikuwa wanadai shilingi 27,250,096 ambapo watumishi wawili tu ndio waliolipwa kwa upande wa Pemba

Mheshimiwa Spika,Kamati ya PAC inaona kuna haja kubwa kwa Serikali kuwathamini watumishi hao kwa kulitilia mkazo wa haraka suala hili la malipo ya fidia kwa watumishi waliopata ajali kazini kwani hao ni wazalendo, waliovuja jasho kwa ajili ya kuitumikia Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, katika Uwekaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya Serikali, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la uwekaji usoridhisha wa kumbukumbu mbalimbali za kifedha katika Mawizra na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika,kwa mujibu wa kifungu 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016 Afisa Mhasibu ataweka kumbukumbu zinazohusiana na masuala ya fedha za Idara, Taasisi za Biashara au Taasisi za Kikatiba kulingana na masharti na viwango.

Mheshimiwa Spika, katika kuthibitisha uwekaji mbaya wa kumbukumbu za kifedha katika Mawizara na Taasisi za Serikali. Kamati ya PAC ilipata mshangao baada ya kuelezwa na Mhasibu wa Wizara ya Afya Pemba kushindwa kujua kama Wizara yake ina bakaa ya fedha zipatazo 20,000,000 liyokaa hadi muda wa matumizi kumalizika na hatimaye fedha hizo kurudishwa hazina wakati fedha hizo zingetumika kwa matumizi mengine ya Wizara .

Mheshimiwa Spika, Kitendo hiki kimeitia aibu Fani ya Uhasibu kwani kuna njia nyingi za kujua kama Taasisi yako inayo fedha au haina ikiwemo ya kufanya mara kwa mara usuluhishi wa taarifa za Kibenki (Bank Reconciliation) na pia kwa kutumia daftari la kumbukumbu za kifedha (cash book).

Mheshimiwa Spika, katika suala la Ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za Ununuzi, Kamati ya PAC imebaini ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali hazifuati kikamilifu masharti yaliyomo katika sheria ya Ununuzi za na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 miongoni mwa dosari zilizojitokeza ni uundwaji wa Kamati ya tathmini ya Zabuni ulio kinyume na Sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi,Mawasilano na usafirishaji imechukua juhudi kubwa kwa kununua Boti tano za kusafiria katika visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar zenye thamani ya 4,076,535,091 ikiwemo boti ya,Tumbatu, Kojani, Kisiwa Panza, Makoongwe na Fundo ambapo wananchi wameanza kufaidika nazo katika kazi zao za maendeleo na kujipatia riziki, hata hivyo Kamati ya PAC imebaini kuwa kuna kasoro mbalimbali zilizozikumba boti hizo ikiwemo kuchelewa kufika na zilipofika zimechelewa kutumika kwa kipindi cha muda mrefu kwa mfano boti ya Mkokotoni hadi Kamati ilipokwenda kuikagua mwezi wa Januari 2022, ilikuwa bado haijaanza kufanya kazi isipokuwa siku moja tu ilipowapeleka Wananchi katika Maulidi ya Tumbatu.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mfumo wa IFIMS Ofisi ya Raisi Fedha na Mipango imekiri kuwepo kwa Dosari za mfumo wa IFIMS kama zilivobainishwa katika Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa mwaka wa fedha unaoishia

tarehe 30 Juni 2020

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ya PAC imefarijika kuona kuwa baadhi ya Dosari zilizobainika katika Ripoti hiyo ya Ukaguzi zimeanza kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na mpango wa Serikali kutaka kuanzisha Mfumo mpya wa Bajeti na Matumizi (BAMAS) ambao utatatua dosari zilizopo za Mfumo wa IFIMS

**Mheshimiwa Spika,** katika Uchunguzi wa Hoja zilizomo katika Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Magizo ya Mhe.Rais kuhusu Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Pemba Kamati ya PAC imebaini mambo ya msingi ambayo yamepelekea kuwepo kwa dosari zilizoainishwa katika ripoti hiyo ikiwemo mikopo ambayo haikurudishwa shilingi 125,654,000.

**Mheshimiwa Spika,**ingawa Wizara yenye dhamana ya Mfuko wa Uwezeshaji imechukua juhudi kadhaa katika kufuatilia urejeshaji wa mikopo hiyo, Kamati ya PAC baada ya kukaa na Watendaji na kufanya ziara na kukutana na baadhi Wakopeshwaji katika wilaya zote za Pemba ili kujua pamoja na mambo mengine sababu zilizopelekea kutokurejesha mikopo kwa wakati, Kamati imebaini mambo ya msingi yafuatayo:-

i. Ukosefu wa Elimu ya UjasiriAmali pamoja na kukosekana kwa wataalamu wa fani zinazohusiana na kazi wanazozifanya Wajasiriamali kwa mfano kazi za kilimo cha mboga mboga ,Mifugo na Biashara

ii. Ufahamu potofu wa Wananchi kuona fedha za Mikopo kutoka Serikalini ni kama sadaka.

iii. Udhaifu wa Mikataba kwa Wakopeshwaji.

iv. Kukosekana kwa soko la uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa na Wajasiriamali.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hayo Kamati ya PAC inaishauri Wizara yenye dhamana na Mfuko wa Uwezeshaji kuwa karibu zaidi na Wajasiriamali kwa kutoa Elimu ya kutosha ya Mikopo na kuwasaidia kuwapatia wataalamu wanaolingana na kazi zao,pamoja na kupatikana kwa soko la uhakika la bidhaa zao ili waweze kufanya

kazi zao kwa tija zaidi.

heshimiwa Spika, kwa upande wa Uchunguzi wa Ripoti ya Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, ni ukweli usofichika kuwa Miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ikiwemo miradi ya maji, elimu na miundombinu ya barabara na umeme inawasaidia Wananchi wengi na kuwaondolea kero mbalimmbali zinazowakabili. Hata hivyo, katika uchunguzi wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo Kamati imebaini dosari kadhaa zikiwemo zifuatazo:-

i. Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri na Mabaraza ya Mji) Kutofanya kazi za Makatibu wa Kamati za Mfuko wa Majimbo kama Sheria Sheria namba 4 ya mwaka 2012 inavyoelekeza hasa kwa upande wa majimbo ya Unguja Mjini, Aidha kwa baadhi Majimbo ya nayowashirikisha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kumekuwa na hali kutofautiana baina ya Wenyeviti na Wakurugenzi hao.

ii. Uchache wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kulingana na changamoto na mahitaji yaliyopo katika majimbo.

iii. Kuwepo Kwa Miradi mingi ambayo haiwezi kutekelezeka kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo ni Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, ni matumaini ya Kamati ya PAC kuwa Viongozi hawa kwa kushirikiana na Serikali watatathimini ufanisi wa utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo na watathmini Sheria na miongozo inayohusika kisha kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mambo yote yaliyobainishwa na Kamati zikiwemo dosari mbali mbali za taratibu za kifedha na Ununuzi pamoja na mapendekezo ya Kamati yamefafanuliwa kwa kina katika Hoja mbalimbali mahsusi zinazozihusu Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali na Majimbo kama zinavyoonekana katika Ripoti yetu. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa Serikali itazifanyia kazi kasoro zote zilizobainishwa na Kamati kwa kuyatekeleza mapendekezo yaliyotolewa, kwa maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kwa namna ya pekee kabisa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako

Tukufu kuwasilisha muhktasari huu wa Ripoti ya Kamati ya PAC kwa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kazi za Kamati ya PAC zinatekelezwa na Wajumbe wa Kamati kwa usaidizi mkubwa wa Sekretarieti ya Kamati inayojumuisha Makatibu wa Kamati na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivyo basi kwa heshima kubwa, naomba kutoa shukrani maalum na pongezi za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati ya PAC na Sekretarieti ya Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya na umakini wao wa hali ya juu waliouonesha bila ya kuchoka wakati wote wa utekelezaji wa majukumu mazito ya Kamati hii hadi tunawasilisha Ripoti hii.

**Mheshimwa Spika**, kutokana na umuhimu huo, naomba kuwataja Wajumbe na Sekretarieti hiyo ya Kamati kama ifuatavyo :-

| | | |
|---|---|---|
| 1) | MHE. JUMA ALI KHATIB | MWENYEKITI. |
| 2) | MHE. SALHA MOH'D MWINJUMA | MAKAMO MWENYEKITI. |
| 3) | MHE. ASHA ABDALLA MUSSA | MJUMBE |
| 4) | MHE. MIHAYO JUMA N'HUNGA | MJUMBE |
| 5) | MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN | MJUMBE |
| 6) | MHE. MARYAM THANI JUMA | MJUMBE |
| 7) | MHE. SULUBU KIDONGO AMOUR | MJUMBE |
| 8) | NDG. HAJI KHATIB HAJI | KATIBU |
| 9) | NDG. MARYAM HAJI ALI | KATIBU |
| 10) | NDG.NASSOR MDACHI MWINYI | MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI- (UNGUJA) |
| 11) | NDG .SALUM SULEIMAN ALI | MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI - (UNGUJA) |
| 12) | NDG .JUMA MOHAMMED JUMA | MKAGUZI- OFISI YA MDHIBITI -(UNGUJA) |
| 13) | NDG.MOHAMAD SALEH JUMA | MKAGUZI - OFISI YA MDHIBIT - (PEMBA) |
| 14) | NDG. SAAD OTHMAN SAAD | MHANDISI WA BARAZA LA WAWAKILISHI |

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikiri kuwa ufanisi wa Kamati ya PAC haushii tu kwa Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati bali pia huchangiwa na mambo mengi yakiwemo uundwaji wa Kamati yenyewe, Uwezeshaji wa rasilimali mbalimbali, Ushiriki, Uratibu, Utoaji wa Mafunzo pamoja na aina nyenginezo za ushirkiano kutoka Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mchango mkubwa uliotolewa na Taasisi hizo katika kufanikisha kazi za Kamati ya PAC, naomba kuzitambua kwa kuzitaja Taasisi hizo kama ifuatavyo:-

i. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.
ii. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
iii. Wizara na Taasisi za Serikali.
iv. Kamati za Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza na ninawaomba waijadili na hatimae kuipitisha Ripoti hii ya Kamati ya PAC kwa lengo la kupata utekelezaji wa Serikali ili kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa mapato na nidhamu ya matumizi ya rasilimali za Umma kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

…………………………….

JUMA ALI KHATIB,

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali

Baraza laWawakilishi,

Zanzibar.